

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA SABA

KIKAO CHA AROBAINI NA MBILI

06 JUNI, 2017



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA SABA

KIKAO CHA AROBAINI NA MBILI – TAREHE 06 JUNI, 2017

I. DUA:

II. MASWALI:

OFISI YA WAZIRI MKUU:

341. **MHESHIMIWA INNOCENT LUGHA
BASHUNGWA (KARAGWE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:- NSSF ilikuwa na mpango wa kutoa mikopo kwa Vyama vya Ushirika ili viweze kukopesha Wanachama wake. Kwa upande wa Karagwe Wananchi walitozwa michango ya kujiunga na NSSF lakini hawajapata mikopo hiyo:-

(a) Je, ni lini NSSF itatoa hiyo mikopo nafuu;

(b) Je, ni kwa nini Wananchi wanailalamikia NSSF kwa muda mrefu lakini hakuna majibu yanayotolewa.

**342. MHESHIMIWA STELLA ALEX IKUPA
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Je, ni lini Serikali itaanzisha miradi maalum itakayosaidia kupunguza ama kuondoa makali ya maisha kwa watu wenye ulemavu wasio na ajira maofisini.

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

**343. MHESHIMIWA OSCAR RWEGASIRA MUKASA
(BIHARAMULO MAGHARIBI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Kijiji cha Nyakanazi Wilaya ya Biharamulo kiko kwenye njia panda kwenda Kigoma, Kahama, Ngara na kina wakazi wapatao 15,000. Kulingana na hali hiyo kuna shughuli nyingi za kiuchumi zinaibuka na idadi ya watu inaongezeka kwa kasi; Aidha, Kijiji hicho pia kimebanwa na Hifadhi inayopakana nacho:-

Je, Serikali ipo tayari kujadiliana na Halmashauri ya Wilaya na wakazi wa Nyakanazi ili kuona uwezekano wa upanuzi wa eneo la Kijiji kwa upande wa Hifadhi inayopakana na Kituo cha Polisi kwa nia ya kufungua fursa za kiuchumi.

**WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA,
WAZEE NA WATOTO:**

**344. MHESHIMIWA SAVERINA SILVANUS
MWIJAGE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:- Serikali ilitoa tamko kuwa watoto chini ya miaka mitano, wazee pamoja na wagonjwa wa UKIMWI na TB watibiwe bure:-

- (a) Je, Serikali imetekelezaje mpango huo;
- (b) Je, makundi hayo yameshaanza kupata matibabu bure kama ilivyopangwa.

**345. MHESHIMIWA PAULINE PHILIP GEKUL
(BABATI MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:- Kuna mkanganyiko wa kutoza ada ya ukaguzi kati ya TFDA na Halmashauri kwa wafanyabiashara wale wale:-

Je, ni kwa nini chanzo hiki cha mapato kisiachwe kwa Halmashauri.

WIZARA WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:

346. MHESHIMIWA VENANCE METHUSALAH MWAMOTO (KILOLO):

Atamuuliza Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo:-

- (a) Je, kuna wachezaji wangapi wa nje wanaoruhusiwa kucheza kwenye Ligi Kuu Tanzania;
- (b) Je, tulianza na wachezaji wangapi miaka ya nyuma na sasa wako wangapi;
- (c) Je, ni zipi sababu za kuongeza au kupunguza wachezaji na ni nini manufaa yake.

WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:

347. MHESHIMIWA JOSEPH GEORGE KAKUNDA (SIKONGE) :

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:- Upembuzi yakinifu kwa ajili ya kuijenga kwa kiwango cha lami barabara ya Ipole – Lungwa ulianza miaka mingi iliyopita na hii ni sehemu ya barabara kuu (Trunk Road) inayounganisha Makao Makuu ya Mkoa wa

Tabora na Makao Makuu ya Mkoa wa Mbeya. Katika Mwaka wa Fedha 2016/2017 barabara hiyo ilitengewa shilingi 350,000,000 kwa ajili ya kumalizia upembuzi yakinifu na usanifu wa kina:-

Je, ni lini barabara hiyo itajengwa kwa kiwango cha lami.

348. MHESHIMIWA EZEKIEL MAGOLYO MAIGE (MSALALA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:- Ilani ya CCM 2015-2020 imeelekeza kwamba Serikali itajenga kwa kiwango cha lami barabara inayounganisha Mji wa Kahama (Manzese) hadi Geita kupitia Mgodi wa Bulyanhulu na upembuzi yakinifu ulishakamilika na Mheshimiwa Rais katika ziara yake aliahidi ujenzi huo kuanza mwaka 2017/2018:-


- (a) Je, ni kiasi gani cha fedha kinahitajika ili kutekeleza mradi huo;
- (b) Je, Serikali imejiandaaje kuanza ujenzi huo mwaka 2017;
- (c) Kwa kuwa mara zote miradi ya Serikali huchelewa kutokana na ukosefu wa fedha; Je, Serikali imewashirikisha wawekezaji wa Migodi ya Buzwagi, Bulyanhulu na Geita ili washiriki katika ujenzi huo.

WIZARA YA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:

**349. MHESHIMIWA ALBERT OBAMA NTABALIBA
(BUHIGWE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji:- Katika Jimbo la Buhigwe hususani eneo la Munzeze, soko la zao la Tangawizi limekuwa la shida sana na Tangawizi huuzwa bei ya chini sana:-

Je, Serikali inasaidiaje upatikanaji wa masoko ili Wananchi wauze zao hilo kwa bei ambayo itawafaidisha.



**DODOMA
06 JUNI, 2017**

**DKT. T. D. KASHILILAH
KATIBU WA BUNGE**